



KENYA MARITIME AUTHORITY
P.O BOX 95076-80104, Mombasa, Kenya,
Tel. 020-2381203/ 020-2381204
Email: Info@kma.go.ke/ Rmrcc@kma.go.ke

USHAURI WA HALI YA HEWA

Nambari 04 ya 2021

Tarehe 22 Julai 2021

Shirika la Kenya Maritime Authority (K.M.A), linawashauri wavuvi, wasafiri na wafanya kazi wote wa baharini, kwamba ;

Kuanzia Jumamosi 24 Julai mpaka 25 Julai 2021 Upepo wa kasi ya zaidi ya Noti 20 unatarajiwa kushuhudiwa. Kuna uwezekano upepo huo kuongezeka hadi Noti 40 (20.6 mita kwa sekunde). Hali hii itakuwa ya mawimbi urefu wa mita 3.5 sehemu za Bahari ya Hindi na ufuo wake.

Kaunti za Marsabit, Isiolo, Mandera, Wajir, Garissa, Kitui, Makueni, Taita Taveta, Tana River, Lamu, Kilifi, Mombasa and Kwale ni baadhi ya sehemu zinazokisiwa kuadhirika na hali hii.

Upepo na mawimbi haya yatapungua hadi Noti 20 na mita 2.4 mtawalia Jumatatu tarehe 26 Julai 2021.

Watu kutoka maeneo yaliyotajwa wanaombwa kuwa waangalifu kwani upepo huu mkali unawaeza kusababisha mawimbi makali na kuathiri kuona mbali. Hali hii pia inawaeza kusababisha kuzama kwa mashua na kuhatarisha usalama wa wanaotumia vyombo vya maji.

Licha ya hayo, tunawashauri watumizi wa vyombo vya usafiri majini na wavuvi wote kuwa makini wakati wote na kuendelea kufatilia ujumbe utakaokuwa ukisambazwa muda kwa muda endapo hali itabadilika kiasi cha kuhatarisha usalama baharini.

Ukitataka usaidizi piga simu kwa kituo cha Uokoaji cha KMA (Regional Maritime Rescue Coordination Centre (RMRCC) kupitia nambari za simu: 0721-368313 OR 0737-719414

Robert M. Njue, HSC, 'ndc'(K)
DIRECTOR GENERAL,

Unaweza kuwasiliana nasi kupita anwani zetu: rmrcc@kma.go.ke, prd@kma.go.ke
www.kma.go.ke

Twitter handle: @kmakenya
Facebook: Kenya Maritime Authority